


Ee BWANA UTUONYESHE REHEMA ZAKO.

*Na John Mtui
Nairobi- Kenya*



Ee Bwa na - u tu o nye she re he ma za ko - -



u u tu pe wo - ko vu wa ko



***1. Na nisikie atakavyosema Mungu Bwana,
maana atawaambia watu wake amani,
hakika wokovu wake u karibu na wamchao,
utukufu ukae katika nchi yetu.***

***2. Fadhili na kweli zimekutana,
haki na amani zimebusiana,
kweli imechipuka katika nchi,
haki na imechungulia kutoka mbinguni.***

***3. Naam Bwana kilicho chema,
na nchi yetu itatoa mazao yake,
haki itakwenda mbele zake,
nayo itazifanya hatua zake kuwa njia.***